

CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA



TANGAZO

Jifunze Lugha ya Kichina

Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kwa kushirikiana na Taasisi ya Confucias ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawatangazia wananchi wote kuwa chuo kitaendesha kozi fupi ya lugha ya Kichina itakayoanza tarehe 17/10/2016 Kampus kuu ya MUST-Mbeya. Mwishoni mwa kozi hii, washiriki watakuwa na uwezo wa kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika Kichina. Washiriki hao wataweza pia kuhudhuria kozi za hatua za kati na za juu zinazofundishwa kwa lugha ya Kichina ndani na nje ya Tanzania. Vilevile, kozi hii itawasaidia wale wanaotarajia kusoma zaidi huko China au kufanya biashara, kufanya kazi na makampuni ya Kichina. Kozi hii itafundishwa na waalimu kutoka China.

Kozi: Kichina cha Awali **Hatua:** I, II, III & IV

Mahali: MUST (Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya)

Muda: Masomo ya Asubuhi na Jioni: Miezi Miwili kwa Kila Hatua (Januari-Februari; Mei-Juni; Julai-Agasti, 17 Octoba- 17 Desemba 2016)

Ada: Fomu ya Maombi: Tshs. 10,000/- Ada kwa Kila Hatua ni kama ilifuatavyo kwenye jedwali:

Wanafunzi wa MUST waliosajiliwa/Wanafunzi wa sekondari	Tshs. 120,000/-
Wafanyakazi wa MUST	Tshs. 200,000/-
Watu Nje ya MUST	Tshs. 300,000/-

Malipo yote yafanyike kwenye Akaunti ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia: MTCMEKAZI, Na. 016101002687 NBC, Tawi la Mbeya

PROGRAMMU NYINGINEZO:

- Mtihani wa Umahiri wa Lugha wa Kichina (HSK na HSKK)
- Kambi la Majira ya Joto, Ufadhili wa Masomo na Kufanya Mazoezi ya Kazi Nchini China

JINSI YA KUJIUNGA NA KOZI FUPI

Ili kuweza kujisajili kwa kozi fupi ya hatua za awali za lugha ya Kichina, tafadhali jaza fomu ya maombi ipatikanayo kwenye tovuti ya MUST au Ipatikanayo Chuoni -(Continuing Education Department)

Kwa Maelezo Zaidi, wasiliana nasi kupitia;

Idara ya Elimu Endelevu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya,
S.L.P 131 Mbeya.

Simu: +255 756 442 677 au **0754889796**,

Barua Pepe: mist@mist.ac.tz/contedu@mist.ac.tz